David: Bunge isiwe na kauli ya pamoja ya kujiongezea mishahara na marupurupu mengineo pasipo kuhusisha mkaguzi mkuu wa fedha na mali za uma. Sehemu yangu ya mwisho-ni kuhusu uridhi na upokezanaji wa uwezo, tunapendekeza kuwe na matoke ya uchaguzi wa urais utangazwe mara tu kura zote zitakapo linganishwa kutoka vituo vyote vya uchaguzi. Katiba iwe na uwezo wa kuidhinisha Rais ambaye anaondoka kushitakiwa kama alivunja au kuaribu mali na masilahi ya nchi na pia kama hakukosa apewe ifadhi na marupurupu yake ainayo stahili yeye na jamii yake. Ya mwisho tunapendekeza kuwe na serikali moja kuu ambayo inauwezo kamili wa kukuza demokrasia kulingana na watu wote wa nchi yake ambapo viongozi wana shuhudia. Ni hayo tu.

Com. Adagala: Okay asante, hapa Kennedy yuko? Okay utampata?

Patrick: Katiba yangu ya kwanza, kwanza ni kurudisha shukurani kwenyu kwa kutusikiliza, Katiba yangu ya kwanza ni kuhusu masomo ya elimu ya bure kwa shule za msingi na iwe ya lazima na iwe sheria katika jamuhuri nzima ya Kenya. Kwa sababu janga la umasikini limetuzidi sisi wananchi na tunaendelea kushindwa kuweza kuelimisha watoto wetu katika shule nyingi za msingi.

Com. Adagala: Halo, halo unasoma? Hiyo ni written submission umebakia na dakika nne na usisome itakumalizia wakati. Pendekezo lako.

Patrick: Pendekezo langu ni elimu iwe free kote katika jamhuri zima ya Kenya ili wananchi waweze kupeleka watoto wote katika shule. Pendekezo lingine katika shule ni walimu kupigwa transfer kote katika ka mashule kila mwaka ukipita, ili tuweze kupata na faida. Pendekezo langu la pili kuhusu kilimo, sector ya kilimo, serikali isiseme kuna uhuru kwa sababu sector kama za KCC ziliaribika na wakulima wanauza maziwa yao kwa shilling tano kwa kila lita. Kama sisi tunauza hapa natunapata hasara kubwa, sisi hatuwezi hata kuelimisha watoto. Hiyo KCC iwe irudishiwe wakulima ili waweze kujiendelea wenyewe, ili waweze kuuza maziwa yao sehemu zenye zemewapatia order.

Com. Adagala: Nakuomba utoe pendekezo, kwa sababu itasaidia sana.

Patrick: Pendekezo langu ni kampuni ya KCC irudishiwe wakulima wenyewe ili waweze kuiendesha kama vile ilikua hapo zamani. Langu ya tatu ni mtu akipatiwa ardhi awe na title deed yake, yaani awe na haki ya kumiliki shamba lake, asije akaitishwa pesa zozote kila mwaka tunalipishwa shilingi arobaini na county council, mimi pendekezo langu ningependa katika Katiba kwa sababu mwananchi amepatiwa title deed ili amiliki ardhi yake asiende tena kuitishwa pesa zisizo halali kwa sababu shilingi hizo alikua amelipa na akapewa title deed, ili ukijenga kiosk yako wasije wakaitisha pesa zingine ushindwe na kuendesha biashara yako.

Pendekezo langu la mwisho na ni la tano ni serikali isaidie wananchi kujenga polytechnique schools ili watoto wanaomaliza darasa la nane kwa sababu ni wengi sana walianguka mitihani mwaka huu uliopita, na tunao manyumbani kwa sababu tumeshindwa kuwapeleka secondary schools wako nyumbani na ndio wanazurura hapa kwa sababu hakuna pahali tunaweza kuwapeleka, hakuna polytechniques. Pendekezo langu ni kuweko na driving schools ili watoto hao wa darasa la nane waweze kuajiriwa na serikali kuendesha magari ya serikali.

Com. Adagala: Asante kwa hayo maoni yako. Wakumfuata ni nani? Kennedy?

Kennedy Njenga: Jina langu ni Kennedy Njenga, mchango wangu kuhusu Katiba tunayo nuiya kuwa nayo,

Com. Adagala: Sijui mngenda record ya hapa iwe na hayo manung'uniko yote mnaifanya mpaka miaka mia moja itakayo fika sijui. Tafadhali tuwe kimia mtu aki-present record ya hapa iwe clear, okay?

Kennedy: Mimi maoni yangu kuhusu Katiba, kuna mambo yanayosumbua wananchi katika ka jamhuri yetu nayo ni muundo uliobuni constituencies unaonekana kwa maoni yangu unakasoro fulani maanake uenda ukakuta kuna mtu anawakilisha sehemu iliyo na watu wachache sana hali mtu mwingine MP constituency yake inawatu zaidi ya mara tatu ya mjumbe huyu.

Com. Adagala: Pendekezo?

Kennedy: Pendekezo langu ni constituency ziwe zikigawanywa kuambatana na wingi wa watu. Jambo la pili katika Katiba ilioko sasa, kuna watu waliopigania nchi hii wakijulikana kwa jina la Mau Mau. Hilo lilikua jina la madharau na mimi ngependa katika Katiba inayoundwa sasa Mau Mau walioleta uhuru katika nchi hii wachukuliwe na mambo yao yawekwe katika Katiba ili wakipeleka malalamishi yao yawe niya watu wanaojulikana walikomboa nchi hii kutoka mikononi mwa wakoloni na hawa wa wakati huu hawana heshima hata kidogo hata kwa wale wanao ongoza nchi hii. Sina mengi mimi.

Com. Adagala: Okay mzee unajua watu wamesema, nakuuliza kwa sababu wewe ni mzee makamu, wanasema tufanye constituency kwa population unajua nchi hii watu wengine wanaweza kusema wao wanataka kusafiri kwa sababu watu, wewe mwenyewe unajua kunawatu ambao walikua kwa emergency kama ile ilikua hapa mpaka 1991, hawakua na haki yeyote

hawakua na maendeleo yeyote na pia kuuwawa wameuwawa, wamepigwa risasi. Sasa mjue vitu vingine ni sensitive kuna watu watakaosema kama hatuko kama wale wengine wacha sisi tuwe na nchi yetu.

Kennedy: Maoni yangu si kama namna hayo.

Com. Adagala: Lakini na sema ukisema iendelea kwa sababu unaweza kusema hapa iko over populated yes, na wao waseme wao ndio wamelinda population, wengine wanaweza kusema wao ndio wamechungu uzazi. Nasema tu, sitaki ujibu lakini mjue mkisema kitu kuna opposite views, so if we are going round there will be opposite views, there will be some other people who will say they think they have been denied this, so they should get it. Kama vile wamekua denied barabara na wale ambao walipata wasipate. Even this things of education, watu wanasema sehemu zingine walikua na nafasi 1960, 1970, 1980, 1990 sasa it is there turn to rebuilt schools so that they can be on the same level. Okay. Am not saying sikuandami wewe lakini nasema tukisema vitu pia tujue kuna watu wako kwa hali tofauti, kama hii ya population kwa constituencies ni sawa, kwa sababu tunasema hapa kwa sababu tuko watu wengi. Wale wako kwa sehemu ya watu chache watesema yao. Naikifika national Constitutional forum itakua na majadiliano na hii takuwa imesema iwe popullation na wale watasema lakini sisi hatuna population kwa sababu hatukuwa na development, vitu kama hivyo, hiyo ndio majadiliano itatokea baadaye. Ili tusione ile tunasema ndio itakua au inaweza hata kuwa na wengine waseme iaendelee hivyo hivyo. Okay.

Kennedy: Kitu kinachofanya niongee na namna hiyo ni kwa sababu yule mtu anawatu kidogo akiwaita mara moja wanakusanyika na anawashauri vile mambo yanavyoendelea endelea. Nafikiri mwingine akiwa na watu wengi anaweza kufanya mkutano ata wiki tatu kabla haja kusanya watu wake wote.

Com. Adagala: Yule ambaye hako na watu wachache atakwambia lazima na nimeona hiyo kwa sababu nimetoka sehemu kama hizo last week, anaenda 100 miles. Kuna constituency zingine ziko 300miles across like that, sisemi ni vibaya itakua na balance kwa national Constitutional conference ambayo itakuweco na watu wote watakusanywa watu mia sita tulisema hii asubuhi, lakini watu wengi hawatakuweco, sasa yote yatachanganywa na watu watakua wakijitetea, wewe unajitetea hapa sivyo? Yah lakini pia kuna hiyo itatokea wakati huo. Kujitetea itakua aje? Na sio kusema hii haitakubaliwa kwa sababu watu wakiwa wengi, ni watu wengi watu wakiwa wachache ni watu wachache. Haya.

Com. Adagala: Daniel Kamau, Alex Kimondo, Ngao yuko? Itika kama uko, ako wapi? simama uje mbele. Jessy Muturi, kamora, Peter Kamora, Kavata haya njoo.

John Gitau: Jina ni John Gitau,

Com. Adagla: Mpeni mzee heshima, tafadhali, office ya officers hallo, George mpeni mzee heshima tafadhali.

John: Mine is on the side of farmers in Kenya, a farmer should have a say on his crops. when selling his crops in the market his money should come directly to him, a go between person should be avoided in handling this money. On the side of co-operative societies, they should revived our KCC, KFA, BBK and many others should be there so that our youth can get employment there.

About administration, we have an assistance chief, chief, DO, DC, PC they should be appointed and interviewed by the Public Service Commission. On education there should be a free education from nursery to standard eight. Also when a child leaves form four to my view there should be one year either in the university for discipline and more learning on human relationship because his degree will depend on the nation. There are some ministries which should be given maximum support by the government, these are ministry of health, ministry of agriculture and veterinary department because most of our people rely on that.

Also we have our natural resources, these are mines, we have places in Kenya where mines are mined, we have our forest we have animals where our tourists come and pay lot of money to the country. All the money collected should be drained in the government revenue because it is from this place where this money will be distributed to the country. Employees seekers on the side of administration, parastatals, co-operatives, these people should be trained personnels to handle this post. Also people in the education sector seeking employment through Public Service Commission should be qualified and their academic qualifications merited. We have animals in the national parks and reserves, these animals sometimes destroy our crops and also they kill people, the law of compensation should be applied immediately.

Powers of the Executive should be trimmed, that is office of the President. We have citizens who live as squatters, some live in the slums, some on the road sides, they should be accorded with health care, shelter, clothes, water, food and amenities as basic needs. The government should look at that. On the side of electing the President, he should be a holder of a degree in economics, political science, all those two tied with a diploma in theology. We have also some maps in the Ministry of Works which show that a certain roads in Kenya or some places are tarmacked, but when you go physically to this places the road are not tarmacked. The new Constitution should look at that because the citizen is the sufferer.

Also we have women's rights, disabled rights and the children rights, these should be observed very highly in the Constitution. On the other side we have retirees, on this issues I take teachers, once they retire after the age of 55 there some things removed to them these are National Insurance Hospital Funds, House Allowance and it does not mean when such a person goes home at that age he grows young, no he grows old. Therefore, these things should be there. National Insurance Hospital Funds, House Allowance and some other amenities that the government can look at because the person has served for the nation for 30 or 40 years. All that is enough for me.

Com. Adagala: Thank you very much mzee we are satisfied. Okay nani anafuata? Ngao yes, Ngao endelea.

Ngao Maruru: Kwa jina naitwa Baroc Jai Ngai. I propose Executive powers to be shared as follows. We shall have a President who will be incharge of Parliament and the cabinet. We shall also have a chief minister....

Com. Adagala: Excuse me a President who is incharge of?

Ngao: The government, put it as well as Parliament.

Com. Adagala: I want you to say it clearly because you are saying government and then you say Parliament.

Ngao: Parliament and Cabinet.

Com. Adagala: How shall he be incharge of Parliament?

Ngao: MP's shall be under him, we shall also have a chief minister who will be incharge of justice, Prosecution that is AG Chambers, the public service Commission and the office of the Controller and Auditor General. We shall also have deputy chief minister who shall be incharge of security and defence. We shall have a Prime Minister who shall be incharge of local government. All these shall be elected directly by the people but they will not be MP's. On the side of Parliament I propose in the next general election, since in my view, I feel we have too many Parliamentarians, I propose each Parliamentarian should occupy a minimum of 3000sq Km and a minimum population of 150,000, maximum population 450,000 this expects the population of Kenya to stabilize at about 52m in twenty years to come. On the side of elections, counting of the ballots should be at the polling station and the result relaid to the Electoral Commission at district levels.

On nationality, ID's should be issued when one is leaving secondary school, incase he will not have gone that far they should be given through the councillor. I propose to have chiefs, DO's, and DC's responsibilities taken over by elected leaders, these are councillors and MP's politics must be fully liberalized where by there is free entry and free exit . MP's must be accountable to their electorates and not to there political parties.

Com. Adagala: can you speak alittle faster so that we can give other people time.

Ngao: Electorates must have the power to recall their MP's incase they do not legislate in their favour. The economy should be fully liberalized, no act of Parliament should be passed to prevent any controls in the economy. Monopolies and duopolies, law must be enacted to make them produce goods and services at international prices and quality.

On the issue of land, I propose that it should be under the state but leads to citizen. The new lease money go to benefit the councils which shall be used to run the health and education sectors.

Com. Adagala: Tha was you last submission.

Ngao: My last submission on the side of forests, they should be fully liberalized (inaudible) the paid to the council.

Com. Adagala: Can you please stop now so that other people can have a chance because you are playing there.

Ngao: Okay.

Com. Adagala: Muturi, Muturi, Kamura and Kavata? Okay.

Peter Kamura: Kwa jina Peter Kamura. Yangu ya kwanza naaza na Rais, Rais hasiwe na mamlaka ya juu. Mamlaka yake yawe yakichunguzwa na Parliament. Ya pili wabunge wetu wakichaguliwa wawe wana fungua office kila location tuwe tukijadiliana nao. Ya tatu hospitali iwe ni free bila malipo, hizi hospitali za private ziondolewe kwa vile tangu hospitali za private zilianza zikawa nyingi ndio matibabu yakawa ya gharama nyingi,. Kwa hivyo private hospital ziondolewa.

Ya nne, schools, tangu wakati tulianza kuwa na school za private, shule za serikali zikarudi chini kwa hivyo private schools ziondolewe. Na ya mwisho wakati watu wanapigania viti wanaambiwa kila mtu anapigania kiti pahali alikua anafanya kazi awache, a-withdraw kazi kwanza ndio apigania kiti. Sasa akisha kuingia Parliament anachaguliwa kila kazi ikawa ni yake. Sasa maoni yangu ni kuwa mtu alikichaguliwa kuwa mbunge awe mbunge bila kazi ingine yoyote, asiwe na kazi ingine yoyote yangu ni hayo tu.

Com. Adagala: Kuna mama ambaye ako hapa? Hakuna akina mama? Central province hakuna wakina mama? Haya tuendelea. Geoffrey Betini Ngethira, Joseph Ng'ang'a, Julius Mwangi, okay come forward. Njungu Mwangi, come forward, Dickson Ndegwa, Estone Mwangi, mtapatana vile nimewaita niko, Joseph Kiragwa: Sema jina lako.

Julius Chege Mwangi: Honourable Commissioners, my name is Julius Chege Mwangi and I do not have a written submission going to represent myself using Kiswahili language so that everyone in the house can understand. Yangu ya kwanza, mimi ningependa Katiba ya Kenya Rais hasiwe na mamlaka kama vile imekuwa kawaida yake, awe akichunguzwa na wabunge katika Parliament. Awe na kura nusu kila area wanapigania. Plot allocation Committee, imekua ni shida sana maskini kupata plot in all towns in Kenya kwa sababu ya land grabbing.

Mimi ningesema Rais hasiwe na mamlaka ya ku-allocate plots anywhere in the Kenya not even Commissioner of Lands. Unless kuwe na plots zimetangazwa katika the council concerned na kuwe na wazee ambao wameteuliwa kuungana na macouncillors, ambao watakuwa pamoja na land Commissioners ndio maskini apate plot ya kujenga pahali pa kukaa. Kuna haya mambo ya raping of the school girls. Mimi ningesema ya kwamba mwalimu yeyote ambaye ata-rape mtoto wa shule mahali anasomesha au pahali pengine awe well disciplined, afutwe kazi, na alee huyu mpaka mtoto amalize shule. Na if it is possible aende prison kwa sababu yeye ndiye mchungaji wa huyu mtoto.

Com. Adagala: Unasema mtoto yule amekua raped?

Chege: Mtoto ambaye amemzaa huyu mwalimu, amsomeshe kwa sababu hata amemuaribia mama yake wakati. Kwa sababu madam Commissioner ulikua msichana na sasa wewe ni mkubwa, kama hungenesoma hungenekuwa, hapa kwa hivyo lazima watoto wachungwe sana hasa wa kike. There are a group of freedom fighters in this country. Before mkoloni tunaongozwa na wazungu hata sasa hizo positions zenu zingekua na wazungu ama wahindi. Lakini kuna watu walienda msituni walipigana mpaka uhuru ukapatikana but hao watu wamesahaulika kabisa, hata mabibi wa wale waliokufa wanakaa tu bila mashamba, yamegawanywa na hawajakuwa considered. Hata watoto wao hawaja soma. Kwa hivyo ningefikiria Katiba ijao hao watu wafikiriwe. Mambo ya quota system.

Com. Adagala: Mtaketi na msembe vipi watafiliriwa. Only you who fought know how mnataka mfikiriwe the problem ni kwa sababu watu wanawacha jukumu kwa watu wengine, kama wanawake hapa wameacha jukumu kwa wanaume. Watu wachache wanazungumza mambo ya wanawake. Lakini freedom fighters mliachia watu wengine jukumu lenu. Sasa mketi muandike vile kwa sababu mimi siwezi kuelewa shida za freedom fighters. Mtaandika na mtume memorandum ingine sivyo mzee.

Chege: Sawa asante. This quota system ya masomo imehangaisha watoto wengi kabisa kwa sababu kuna mtoto ambaye ametoka province fulani amesoma vizuri na amepita na kuna mtoto mwingine ambaye ako katika province zingine hasomi na wakati mtoto ambaye hakusoma na hakupita vizuri anaenda katika government school na huyu mwingine ambaye alisoma vizuri na akapita hakuenda kwa sababu ya quota system hiyo ningefikiria masoma ya shule yaangaliwe katika merit kama vile mtoto amesoma, amepita vizuri aendeleo kwa sababu katika Kenya yetu ambayo tuko, walimu wanakuwa distributed kwa shule nawamesoma katika shule, moja. It is responsibilities of a teacher to go and teach his people properly, kwa hivyo ningesema allocation, iwe kulingana na vile mtoto amepita.

Com. Adagala: Unajua ubaya wa education atukuwa na usawa wa kugawa shule na vifaa in the 60's, 70's, 80's and 90's Ndio hiyo inaleta halafu, lakini mimi sisemi nakubali au la lakini tufanye aje?

Ngao: Mimi ningefikiria kawa sababu kuna National Schools, hizo ndizo ziko na shida. Watoto wapite na waende kulingana na merit. Kwa sababu everywhere in Kenya there are schools na hakuna walimu wametumwa wasomeshe na wanasomesha vizuri and there are all in one grade, hata hapa kwetu kule kuna shule nyingi kuna shule ambayo haifunzi masomo vizuri kwa sababu walimu wanakua reluctant. Kwa hivyo ningesema shuleni watoto wachukuliwe kulingana na vile wamepita. Mambo ya defectors, kama MP amedefect kutoka chama hiki na kingine na au councillor amefanya hivyo ningesema ya kwamaba kuna mbunge wa chama hicho ambaye alikua second, baadala ya kuhangaisha wananchi kwa kuchaguana na kutumia pesa nyingi za serikali yule aliyekuwa wa pili achukue hiyo nafasi.

Hii mambo ya landless Tumeona ya kwamba pengine hata serikali imejaribu kutafuta ardhi ya kupatia landless, Tumeona hata pengine wanachukua sehemu fulani wanawapa lakini katika Kenya yetu kwa sababu ya corruption, those who really have needy cases wale hawana shamba, hii shamba, linachukuliwa na wakubwa hata kama ni Member of Parliament, hata kama ni Ministers na wa kubwa wanenda wanachukua hizo shamba nawanaenda nazo. Zingine wanasema wanapatia wale waliowachagua. Katika Kenya hata kama ulichaguliwa na watu lakini hata wengine walichagua wengine. Na hakuna Kenya mbili na hakuna Kenya ya wengine. Kwa hivyo kuwe na kamati ambayo itachunguza land allocation tu-jue the needy cases ambazo zitafanya hawa watu wapate land, lakini sio yule mtu ako na 100ha., 1000ha, anapatiwa anaenda kuuza.

Earlier on nilikua nimeongea mambo ya rapes of school girls. Mimi sasa ningependa kuongea in general mambo akina mama wote. It is bitter enough ya kwamba wa mama wetu wanakua raped, wanafanyiwa kama kinyama, they should be well respected kwa sababu wao ndio pia wanatuzaa. Yule atakayepatikana na kesi hiyo ya kurape any woman, awe nikama yule aliyeiba with violence apate kiboko ya kutosha na apelekwe katika prison, na ikiwezekana kama ni mbaya sana anaweza kunyongwa. Kina mama must be respected kwa sababu hao ndio walituzaa likani wanafanyiwa na sisi wanaume kinyama kabisa. You meet with her you rape her and on.

Upande mwingine ni Judiciary upande wa kotini. Unaona hata kama mwingine ameiba na amepatikana na vitu ambazo ameiba lakini bribes zinapelekwa kotini na huyu mtu anakuwa released mimi ningesema any magistrate ambaye atakua involved in such cases afutwe na afungwe. Madam Commissioner ningesema serikali ya mbele kabisa hata ya jusi kulikua na pesa tasilimu za serikali ambazo zilikua zimepakwa rangi ukiguza na namna hiyo nikiku-bribe na CID watakua wamekufuata, hata ukieka na upelekwe katika laboratories utapatikana uliuguza hizo pesa. If corruption is not from our big fish in the country, mimi ningesema hizo pesa zirudi kwa sababu nikiwa nimekuonga surely nimekupatia pesa kwa mkono tasilimu na utafuatwa na CID na utashikwa na hizo pesa lakini the problem hata CID huyu atakufuata naye ni corrupt naye pia atapewa pesa atakuacha. Nunakuja upande wa police.

Com. Adagala: Hio iwe ya mwisho mzee.

Ngao: Mimi ningesema mambo ya polisi wawe wakiajiriwa baada ya kupata recommendation kutoka kwa chifu na kwa wazee kwa sababu wakati polisi wanapelekwa katika district yetu ya Nyahururu mtu anatoka pahali anatoka na pengine aliwa mwizi na anajiriwa na akipelekwa katika kikosi cha jeshi anafundishwa sasa kupiga risasi, hao ndio wanatoka huko wanachukua bunduki wanakuja kupiga wazee na kina mama usiku kwa nyumba. Kwa hivyo ningefikiria kwamba kila mtoto ambaye ataajiriwa katika police leave alone jeshi awe na recommendations kutoka kwa chifu na kamati katika location ndio sasa ijulikane ya kwamba huyu mtu ni mzuri na huyu mtu akienda afanye makosa hiyo report itarudia huyu chifu.

Hizi pesa za Kenya au za nchi zingine tunatumia pesa nyingi sana kwa kila President, sasa tulikua na Kenyatta zitageuzwa

zikawa za Moi, tukakua na mwingine, tukakua na mwingine, I think we are spending a lot of money kutengeneza pesa zenye picha ya President. Mimi ningefikiria iwe ni either Moi au kenya, wale Presidents wote watakuja, zote ziwe na hiyo picha yake. Tutumie pesa moja tu katika jamhuri ya Kenya. Tusitumie pesa nyingi bure. Niyo tu.

Com. Adagala: Kunasheria ya pesa nikama kumbu kumbu hiyo portrait. Sasa mheshimiwa alisema kwa nchi zingine inajukua miaka hamsini ndio inawekwa hiyo, ni kama kumbu kumbu sio kuweka watu wambao wamefariki juzi au wale wako hai. Hapo ungesema aje?

Ngao: hapa ningesema katika Bunge hiyo sheria ipelekwe katika Bunge ikaguliwe na wa -bunge.

Com. Adagala: Umesema vizuri kwa sababu vitu vingine vinafaa viende Bunge. Haya ni nani anafuata kamura, jina lako

Henry Wanjohi Timothy: Jina langu ni Henru Wanjohi Timothy, na mimi nataka kuzungumza juu ya mambo matatu ambayo mimi naona yanapaswa kurekebishwa. Ya kwanza: kuna sheria moja ambayo ilikuwa hata zamani hata wakati wa ubeberu. Na Sheria hiyo ni kuhusu shamba, ati ya kwamba mtu akija kwangu aniulize nimpatie mahali pa kukaa tukae naye kwa mda mrefu kama zaidi ya miaka kumi. Wakati ule mimi nitamwambia ati yeye sasa ni vizuri aondoke, sasa yeye inakua ni ngumu, tunarururtana na yeye. Tukienda kotini sasa yeye huko anambiwa kwa sababu nimekaa na yeye lazima ni mpatie sehemu ili aweze kuishi. Hiyo sheria mimi naonelea ya kwamba itolewe kwa sababu hiyo inaleta ugomvi hiyo inaleta chuki na wakati yule mtu akaniuliza kwa hiarinilimpatia kwa uzuri, lakini nikimuuliza aondoke kwangu sasa inakua ni shida. Hiyo sheria ifutwe kabisa kwa sababu inapiganisha watu hata kuuana watu watu wanauaana kwa sababu ya mambo kama haya. Hiyo ni moja.

Ya pili ni mila za watu, kwa sababu kila watu wako na mila zao, ningependa kwamba hii mila ziwachiwe watu wenyewe wawe wakijitengenezea wakijikatia wenyewe. Kwa sababu mila zetu zikiingizwa kwa mila zingine bila kuwa na hiari, hiyo inaleta mzozo au mgogoro. Kwa hivyo hizi mila ziwachiwe watu wenyewe lakini kile kitu ambacho watakuwa wao wenyewe waone ya kwamba haifai watawacha wenyewe. Kitu ambacho kitafaa sana ni elimu ili waelimishwe na elimu itamaliza hayo maovu yaliyo kwenye mila zingine.

Ya tatu, ningependa kuzungumza juu ya soko huru: Soko huru ni jambo ambalo tumeletewa na wale watu ambao hawajaelimika, hawaelewi soko huru ni nini. Walikua wakifikiri ya kwamba soko huru itawaletea utajiri kwa sababu kila mtu atauza mali yake vile anataka. Sasa imegeuka, badala yakupata utajiri imegeuka ikawa ni umaskini, watu wamezoroteka kabisa.

Kwa hivyo mimi napendekeza ya kwamba kabla watu hawajaleta vitu fulani au mambo hawajui wawe wakielimishwa kwanza ili wajue chenye wanaenda kufanya, hivyo ndio tuondoe umasikini. Ningependekeza kuwe na price control hasa kwa mambo ya mashamba, ile chakula na mambo mengine ambayo yanatumiwa na mwananchi wa kawaida. Hiyo ningetaka serikali

isimamie kwa kuweka price control ili watu wasiweze kufilisika zaidi. Hilo naonelea ni jambo nzuri liwekwe kwenye Katiba. Na kama wanataka kupendekeza kitu fulana au kuingiza kitu fulani waelimishwe kwa sababu watu wanaingizwa kwa mambo hawajui halafu tena yanawaumiza. Hayo yangu ni machache tu. Asanteni sana.

Com. Adagala: Asante umechanga mambo mhimu na ni vizuri. Nani anafuata huyu mzee? Nani huyu? Jina? Asante mzee enda uandikishe hapo. Are people coming to register.

Cllr. Joseph Kariuki Ng'ang'a: Kwa majina yangu kwanza ni councillor Joseh Kariuki Ng'ang'a ambaye anawakilisha ward hii ya Dundori. Kwanza ni kukaribisha -

Com. Adagala: Excuse me, Joseph Kariuki Ng'ang'a. Okay.

Cllr. Joseph: Kwanza ni kuwakaribisha hapa mjisikie mko nyumbani na vile vile kwa sababu sitapata wakati mwingine ngesema wakati wa kuondoka, muondoke salama. Basi pendekezo langu la kwanza ningetaka kuongea juu ya President. President apunguziwe zile powers ako nazo, kwa sababu Tumejionea mambo mengi kulingana na vile tunatawaliwa. Rais ambaye tuko naye anaweza akasema hivi na vile, wakati wowote anaweza akaua, anaweza akakunyang'anya, anaweza akakufuta kazi wakati wowote.

Interjection: (Com. Adagala) Councillor.

Cllr Joseph: Kwa hivyo pendekezo langu ni apunguziwe zile powers zake. Ya pili.

Interjection Com. Adagala) Nataka pendekezo na nitaenda one, two, three. Umesema one, two.

Cllr. Joseph: Nimesema apunguziwe powers zake.

Com. Adagala: Councillor nataka uendelee na uendelee kwa kasi usiwe na maelezo.

Cllr. Joseph: Ya pili ni hali ya local government: Tuko na yule katibu wa baraza, ningetaka vile vile naye apunguziwe powers zake. Ya tatu ni hali ya voters. Wakati wa kupiga kura zile kura tunapiga ziwe zinahesabiwa mahali Tumepigia kura. Hiyo ingine ni juu ya councillors, wawe na population ambayo ni equal, kila councillor awe na jumla ya watu fulani kama ya yule mwingine.

Kwa upande wa elimu ningetaka kuwe na elimu ya bure kuanzia pre-primary mpaka standard eight. Kwa upande wa hospitali ningetaka tuwe na free medical care na tuondoe cost sharing. Kwa upande wa madaktari ningependekeza wapatiwe mishahara

ya kutosha ili tuokoe wizi wa madawa. Kwa upande wa vile mtoto akifikisha miaka kumi na nane inasemekana anachukua kitambulisho na awe ameo. Pendekezo langu ni kua awa amefikisha miaka ishirini na tano na awe ameo.

Interjection: Com. Adagala: Awe amefikisha miaka ngapi?

Cllr Joseph: Awe amefikisha miaka ishirini na tano na awe ameo. Kwa upande wa mashamba kuna watu ambao wako na hekari nyingi katika nchi hii.

Interjection: (Com. Adagala): Pendekezo?

Cllr. Joseph: Pendekezo, ningetaka wale watu tuko nao sana sana vijana, serikali iwapatie angalau mashamba kama heka tano tano hivi. Kwa upande wa street boys and street families.

Interjection: Com. Adagala: Umependekeza nini kwa mashamba?

Cllr Joseph: Nimependekeza kwa sababu watu wengi wako na hekari nyingi, pendekezo ni wale hawana wapatiwe hekari tano.

Com. Adagala: Na juu ya watu wasiwe na mashamba makubwa makubwa, kubwa yenyewe iwe nini?

Cllr. Joseph: Wale wako na mashamba makubwa wapatiwe kama hekari 100.

Com. Adagala: Okay endelea. Iwe ya mwisho

Cllr. Joseph: Kwa hali ya hao vijana au street boys and street families ningependekeza serikali iwapatie mashamba. Kwa upande wa Electoral Commission--

Interjection: Com. Adagala: Hiyo ndio ya mwisho mzee.

Cllr. Joseph: nayo ningependekeza kwa ule mda unaopewa voters, wakati wa kupiga kura uongezwe kama siku mbili au siku tatu. Ni hayo tu, asante.

Com. Adagala. Yule anamfuata ni nani? Niliita majina. Haya nitaenda kwa karatasi ingine basi. Kama hamtaki kuchukua jukumu lenu. Njogu, Dickson, Estone. Nataka muwe hapa mbele mzungumze.

Njogu Mwangi Ngingo: Jina langu ni Njogu Mwangi Ngingo, jambo langu la kwanza kuhusu Katiba ambayo tunatarajia itawale katika Kenya ningesema office ya Rais ipunguziwe uwezo, kwa sababu office ya Rais ndio imekua mashinani ya kuaribu nchi yetu ya Kenya kwa njia ya ufisaidi na mambo yote maovu katika Kenya. Ya pili waheshimiwa .

Interjection: Com. Adagala: Mzee ukichukua mda hivyo tutakuambia uketi.

Njogu Mwangi: Ya pili waheshimiwa ni juu ya uchaguzi wa Rais na kura zote ambazo zitapigwa katika vituo vya kura, viwe vikihesabiwa pale na kutangazwa pale ni nani ameshinda. Ya tatu ningependekeza hali ya uchaguzi kwa upande wa Rais awe akichaguliwa na 51% katika jamhuri yetu ya Kenya kwa-sababu tukifuata ile law ya 12% tunaongozwa na minority. Ya tatu madam kuna watu ambao walijitoa muhanga kwa ajili ya nchi yetu itawale, ningependekeza Katiba ambayo itaundwa iwe ikiwakumbuka kwa sababu walipoteza ndugu zao, baba zao na mama zao kwa ajili ya uhuru wa Kenya na hakuna mahali popote hambapo wanakumbukwa. Ya tatu--

Interjection: Com. Adagala: Unataka wakumbukwe vipi?

Njogu: Vile tunataka wakumbukwe lengo letu tulipo ingia msituni madam tulikuwa na mambo mawili ya mhimu ya kwanza ni uhuru na ya pili ni mashamba. Tulipo pata uhuru madam kuna wakina mama waliopoteza ma-bwana zao na watoto wakapoteza baba zao na hakuna chochote walipata katika Kenya. Uhuru ulipopatikana kile kipawa tungepewa kilipewa wengine. Hali ya masomo ningependekeza ule mtindo...

Interjection: Com. Adagala: Huja sema mzee, umesema maovu, huja sema kile kizuri kinachowafaa freedom fighters.

Njogu: Freedom fighters ningependekeza wale waliokufa na wale walio hai wapewe shamba sababu hilo ndilo lilikuwa lengo lao.

Com. Adagala: Yes endelea.

Njogu: Hali ya mashamba yaliyo katika Kenya madam, kuna watu walinyakua, tunajisumbua ili Kenya ijitawale. Kwa hivyo ningependekeza wale wote wako vijini wapewe angalau heka kumi katika Kenya.

Com. Adagala: Na heka za juu zaidi ziwe ngapi?

Njogu: Yule amezidi heka kumi katika Kenya, kwa sababu wamechukuwa kwa njia isiyo halali serikali ichukue na igawie wale ambao hawana mashamba. Ya tatu Madam mimi naonelea nivibaya sana katika Kenya, wanyama wa mwituni kuishi three quarters ya nchi yetu. Na wananchi wa Kenya ambao ndio hasa wanakenya wanaishi quarter (robo) ya nchi yetu. Ningependekeza

serikali ya Kenya tafadhali iwafikirie wale watu ambao hawana uwezo wowote kwa sababu madam ukirudi hapa nyumbani miratini utawakuta wengine wanaishi kwa 100% na jamii zao madam,

Com. Adagala: Nataka pendekezo.

Njogu: Pendekezo langu ni kuhimiza serikali iwashughulikie tafadhali.

Com. Adagala: Lazima useme vile.

Njogu: Iwape mashamba. Hali ya tatu, wale watu tuko na mashamba hapa Nyandarua tunasumbuliwa na county council ya Nyandarua, kila mwaka wanatuitisha shilling arobaini za shamba na hakuna huduma ambayo wanatuhudumia. Kwa hivyo county council ya Nyandarua ni wasaliti, wanatusaliti pesa zetu bure, ningependekeza hizo pesa ziondolewe. Ya mwisho madam, tuko na taabu ya mahospitali, hospitali zetu za kiserikali hazituhudumii kwa njia nzuri sababu wale wanaotuhudumia katika hospitali zile niwale wameweka dispensary zao huko town. Wanachukua dawa zetu wanapeleka kwa hospitali zao kwa hivyo ukitibiwa pale wanakutuma kwa chemistry fulani ukanunue dawa na zao. Sasa ningependeza yale mahospitali ya private yamalizwe madam na nimemaliza tafadhali.

Com. Adagala: Asante, na sauti yenyewe ni heko. Nani next? Huyu ni nani.

Estone Mwangin Kamau: Mimi kwa majina yangu madam naitwa Estone Mwangi Kamau. Ningependelea mamlaka ya Rais yapunguzwe. Ya pili, ningependelea ushuru uchunguzwe sana na Katiba yetu. Nikisema ushuru namaanisha kama vile tumepewa mashamba na tuna vyeti vya mashamba na kila mtu anaponunua shamba hapa Kenya anatoa pesa za kodi mimi nalipa ushuru wa kila aina na kununua shamba langu lakini ninapo jenga plot kwa shamba langu serikali inaniitisha ushuru? Kila mwaka ushuru na shamba nimenunua ningependa hiyo serikali ichunguze.

Kitu cha tatu ningependa kutaja ni juu ya elimu kwa sababu elimu yetu siku hizi nimeona imekuwa mbaya na chafu sana. Kuanzia mahali serikali iliweka elimu ya nane nne nne, kutoka hapo niliona elimu yetu imeharibika sana kwa hivyo ningesema serikali ichunguze hali ya elimu na vile vile elimu iwe ya bure katika shule za primary. Tena shule za upili ningependelea kama kunawezekana ziwe ni za hali ya kusaidiana malipo. Kwa hivyo iwe ni cost sharing. Lakini shule za msingi ziwe ni bure katika taifa nzima.

La nne ningependa Katiba yetu itusaidie sana kuhusu hospitali zetu. Hospitali za private, mimi kwanza ningependelea ziondolewe zote kwa sababu hapa kwetu Milangini tuko na hospitali na nizaati kidogo hivi, ni nzuri sana na afya yake ilikuwa ni nzuri lakini zile zingine ziko area hii zinatusumbua sana kwa kua ufisadi uko ndani hizo.

Tena kile kitu ningepedelea niutawala kutoka PC hadi kwa chifu. Nikisema hivyo na maanisha Rais wetu hasiwe ndiye anayemteua PC na vile vile DC na DO. Kuwe na Commission inayomchagua PC na ili Rais asiwe na nguvu kuhusu PC na vile vile kuhusu DC na tena machifu pia kama mimi ningeulizwa kama mimi ningeulizwa pendekezo langu ni wawe wakichaguliwa na wananchi, kwa sababu wale wanachaguliwa hatuwaamini wengi wao kama ni wema kwa hivyo mimi pendekezo langu ningependekeza wawe wakichaguliwa na wananchi wenyewe. Tena juu ya wajumbe wetu ningependelea wawe wakichaguliwa na wananchi wanaenda Bunge nao wanachaguwa Commission kama hii yenu, kuliko mtu awe akiichagua kama Rais hivi, ama ati mezani hivi ziwe zikichaguliwa. Na mimi naona tena civil servants wote Katiba itengenezwe kama kikundi ambacho kitakuwa kikichunguza wafanyi kazi wote wa serikali kutoka may be mwalimu mpaka Rais. Kwa maana kwa mfano, vile tuko naona kama hapa kwetu wakati wa kupewa kitambulisho kuna shida kubwa sana, kama vile tumesema hapo mbeleni kama kuitishwa pesa wakati wa kuchukua kitambulisho huo ni ufasidi na unafanywa na machifu wenyewe na hao ma-commissioner kwa sababu wakiweka mia tatu, mia nne, mia tano hiyo ni pesa yao sio serikali, na kama kuna kikosi ambacho serikali imeandaa ama Katiba yetu imeandaa ya kuchunguza civil servants wote itakuwa ni vizuri ufasidi utapungua kidogo hiyo ndio maoni yangu madam.

Com. Adagala: Asante sana mzee umeenda kwa mda mzuri. Nani anafuata? Nani huyu? Jina, nafikiri wakati wako haujafika. Kuna Joseph Kragu, Nicholas Wabungu. Endelea. Joseph Kiragu yuko?

Nicholas Wabungu: Kutoka tulipo pata uhuru mwaka wa sitini na tatu walio pigania uhuru wakapigwa na wazungu na baadaye wakati tulipo pata uhuru, excuse me, tukasahauliwa, tukawa kama sijui nini. Kwa hivyo ningewaomba Commission yenu itufikirie tupate mashamba, watoto wetu wasaidiwe kwa sababu Tume kua masikini kutoka wakati huu. Jambo lingine.

Com. Adagala: Watoto wasaidiwe vipi?

Nicholas: Wasaidiwe wapewe mashamba, kwa sababu hawa ndio tulikuwa tukipigania. Na walimu pia wapewe.

Interjection: Sasa mzee wao ni watu wakubwa sasa?

Nicholas: Ni wakubwa, watoto wetu ni kama wewe na hata huyu, wapate mashamba.

Com. Adagala: Umeongeza na elimu ndio nikakuuliza.

Nicholas: Halafu hapa nikasema, nikirudia upande wa elimu sasa, elimu yetu ya msingi iwe free na hata ikiwezekana kama serikali ina uwezo kwa sababu nilisikia ya kwamba kodi ya serikali ni kubwa sana, wanapata kama billion mia tatu, wakiweka shule yetu free mpaka university ili mtoto wa MauMau kama mimi asome. Kwa sababu hatapata elimu. Mimi niliacha masomo, nikawekwa kuzuizini au nikaenda msituni kupigania uhuru, sasa mtoto wangu kwa vile niliwachwa nikawachiliwa na sikufikiwa

mtoto wangu mpaka leo ni masikini, kwa hivyo ningependa hao watoto wetu waliopigania uhuru wafikiriwe. Tulipigana, mpira ukapewa wale hawakushinda. Kwa hivyo ningeomba Commission yetu ifikirie sana hali hiyo.

Pia ningeomba hao maoni yangu kuhusu afya yawe, mahosipitali yetu yawe free pia. Kwa sababu wale watu masikini kama sisi waliopigania uhuru na wakatupwa nje hawawezi kujimudu kwa upande wa matibabu, wanakufa kama mbwa, anavurutwa tu kwa nyumba anawekwa nje kwa sababu hana mtu wakumsaidia.

Jambo lingine vijana wetu, sasa naingia kwa nchi nzima. Vijana wetu wafikiriwe kwa upande wa mashule ya kuwaelimisha, akianguka mtihani wa standard eight na hata wale wameelimika wapewe kazi. Kwa sababu wakikosa kazi ndio hao wakipigana usiku, kupiga wazee kama sisi. Wanatafuta bunduki wanatukuta usiku kwa sababu ya ukosefu wa kazi kwa hivyo serikali yetu iwafikirie hao vijana wetu. Wasichana kwa vijana. Kuhusu mashamba, mtu akimiliki shamba lake hana haki tena kufuatwa, kumiliki ni kupata title deed, kwa hivyo county council isinifuate nikienda biashara. Makanisa yetu. Kwa upande wa makanisha jambo ningelizungumzia serikali yetu itoe uhuru wa kuabudu ndio, lakini kuna makanisa kama ya shetani ya kuomba hao wanaitwa, sijui wanaitwa nini kwa kingereza mnisaidie?

Interjection: Devil worship.

Nicholas: Yes makanisa kama hayo yaondolewa kwa orodha, na hata mungiki ndio makanisa na ndio sababu najua mungiki hiyo inaleta vita ndani yetu na ndio nasema wapatiwe kazi na serikali, iwafikirie hao vijana wetu, ifikirie iwapatie kazi kusudi wawache kufanya mambo ya ukora ukora, kama huo wa mungiki. Mahakama iwe na uwezo. Ikiwa mahakama imeamua kesi ya kwamba utanyongwa unyongwe sio kungoja Rais hasiwe na uwezo zaidi, hasiwe above the law, sijui kingereza mnasema namna gani. Awe chini na mamlaka mengi ambayo anafanya katika nchi yetu sasa for example Moi na Kenyatta, wamekuwa amri jeshi nao hawajasomea uanajeshi. Inatakiwa yule atakayekuwa amri jeshi mkuu awe generali ambaye ameitimu, sio yeye. Kwa sababu akiwa na madaraka hayo anauwezo wakusema Kenya serikali ipinduliwe tuanze kupigwa bure kwa sababu anauwezo. Kwa hivyo jeshi liwachiwe mamlaka yake.

Haya upande wa elimu, nina moja, kuhusu mamlaka hayo ya Rais. Kupeana degree mtu asiye na degree hana haki ya kupeana degree, hiyo ni aibu. Mimi najua nyinyi mko mbele yangu mumeitimu na mtu ambaye anakupea degree hajaitimu, hii ni aibu tupu kwa nchi yetu na kuna wale ma professor wetu kwa hivyo ningeomba awe chini ya amri. Akitaka kwenda kutembea aombe ruhusa kwa Bunge. Asante sana.

Com. Adagala: Nani anafuata huyu James Kimani, James kimani yuko? Okay, Dick? Endelea.

Allan Kamau Benson: Yangu madam, nikusema mtu akubaliwe kuishi mahali popote bila kutatitika akiwa na security ya kutosha. Hiyo ni maoni yangu ya kwanza. Katika nchi yote pahali ataweza kua, akinunua plot akiwa pahali popote, aweze

kuwa na security ya kutosha ya kuishi popote. Ya pili naongeza kama vile wenzangu wamesema Rais hasiwe na mamlaka makuu, yaani mamlaka yake yaweze kufupishwa. Hiyo ni yangu ya pili. Ingingine ya tatu, waliojipatia mashamba makubwa makubwa tunaona wengine wako na shamba kama hekari mia tatu na hata zaidi na tunaona ma-squater ni wengi sana kwa hivyo maoni yangu ningeeomba mashamba yale yaweze kufupishwa, mtu awe na kama heka mia moja, yule alikuwa na zaidi, ili wale ma-squatters wawe na kama heka kumi ili masikini wawe kidogo kigogo katika nchi yetu, Maana hata wao ni raia wa Kenya. Ingingine ya nne ni kuhusu wanawake, maoni yangu ni katika kitabu, katika bibilia haifeso tano na mistari wa ishirini na tatu mpaka ishirini na nne. Inasema ya kwamba mwanamke awe chini ya mwanaume na ningeeomba maoni yangu ya kwamba, ni vyema hata wanawake wapewe mamlaka ili yaweze kujimudu kimaisha. Lakini wakifika kwa nyumba hasiwe ni kama anamtawala mwanaume kwa ajili ya vile mungu amesema. Kwa maana mungu ameona mwanamke awe chini ya mwanaume, lakini ningeeona yeye apewe madaraka ya kutosha kama Katiba ikiandikwa, lakini kwa wakilishi kwa nyumba awe ameolewa hasiwe na mamlaka zaidi hata ya kuwa akimtawala mwanaume hayo si mapenzi ya mungu kwa hivyo ningeeona Katiba ikiandikwa iweze kuguzia kitabu hicho cha Haifeso tano mstari wa ishirini na tatu mpaka ishirini na nne ili wawe wakikumbuka hayo. Yangu ya mwisho sitakuwa na mengi sana, nafikiri yangu nimemalia asante sana.

Com. Adagala: Okay ndio wanawake hawako hapa kwa sababu mambo hayo yalitangazwa kwa kanisa na wakaona wafuate jambo la mungu.

Com. Salim: Soma majina ya wale ambao wamejiandikisha na ambao bado hawajatoa maoni, na pia ikiwa wako wale ambao wanadai kwamba walijiandikisha lakini hawakusikia majina yao tujue. Sawa?

Com. Salim: Kwanza James G. Kimani?

